TANGAZO LA SERIKALI NA. 351 la tarehe 10/05/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA VIWANDA MBEZI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Viwanda Mbezi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji(mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango

3. Mipango kina katika eneo lililotajwa chini ya aya 2 itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 351 (Linaendelea)*

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YH 756 yenye majira – nukta 522140.638MS, 9259920.015KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YK120 yenye majira - nukta 522215.501MS, 9259983.048KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.15 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YK119 yenye majira - nukta 522310.172MS, 9259859.083KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YF308 yenye majira - nukta 522229.991MS, 9259800.627KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazin - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.15 hadi ulipoanzia".

Dodoma
25 April, 2024

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*